

SHULE YA MSINGI DAISY
S.L.P 1485-50100
KAZI YA DARASA LA NANE 2020.
VIELEZI

- *Hufafanua Zaidi kuhusu vitenzi au vielezi vingine.yaani,hutoa maelezo Zaidi kuhusu vitenzi au vielezi vingine.*
- *Hueleza kitendo kilifanyika lini,wapi,vipi,mara ngapi au hali gani.*
- *Sana sana vielezi huja baada ya kitenzi katika sentensi.*
- *Vielezi vimegawanywa katika mafungu matano.*
 1. Vielezi vya namna/jinsi
 2. Vielezi vya wakati
 3. Vielezi vya mahali
 4. Vielezi vya idadi/kiasi
 5. Vielezi vya kitilia mkazo

(1)vielezi vya namna/jinsi

- Huonyesha jinsi kitendo kilivyofanyika au kilivyotokea.

Mifano ya vielezi:

- ❖ Vibaya
- ❖ Aste aste
- ❖ Chapuchapu
- ❖ Hanga hanga ❖ Harakaharaka ❖ Jii!
- ❖ Kiajabu
- ❖ Kifudifudi
- ❖ Kwa furaha
- ❖ Kwa kuogelea
- ❖ Kivivu
- ❖ Ghafila
- ❖ Juu juu
- ❖ Kijinga
- ❖ Kikatili
- ❖ Kimoyomoyo

- ❖ Kwa gari ❖ Kisirisiri
- ❖ Hobelahobela n.k

Mifano katika sentensi:

- a. Anacheka ***kitoto***
- b. Mkulima alilima ***polepole***
- c. Walisafiri ***kwa gari***
- d. Mpiga mbizi alizama ***zi!***

Kumbuka:vielezi huja baada ya kitenzi au kielezi kingine.

(2)vielezi vya wakati

- Huonyesha wakati wa kitendo kufanyika.Hujibu swali lini.

Mifano:

- ❖ Kesho
- ❖ Jioni
- ❖ Asubuhi
- ❖ Usiku
- ❖ Mtondo ❖ Alasiri
- ❖ Saa saba
- ❖ Mwezi ujao
- ❖ Jumapili
- ❖ Leo
- ❖ Mapema
- ❖ Mchana
- ❖ Punde tu
- ❖ Karibuni
- ❖ Juzi n.k

(3)vielezi vya mahali

- Huonyesha mahali kitendo kilifanyika.Hujibu swali wapi.

Mifano:

- ❖ Angani
- ❖ Darasani
- ❖ Juu

- ❖ Katikati
- ❖ Kando
- ❖ Dukani
- ❖ Chini
- ❖ Mashariki
- ❖ Nje
- ❖ Mbali
- ❖ Karibu
- ❖ Ndani
- ❖ Kwa
- ❖ Msalani
- ❖ Sebulei
- ❖ Uwanjani n.k

(4)vielezi vya idadi

➤ Huonyesha kitendo kimetokea mara ngapi.Hujibu swali ngapi.

Mifano:

- ❖ Daima
- ❖ Kiasi
- ❖ Foko
- ❖ Mara nyingi
- ❖ Mara kumi
- ❖ Mara kadha wa kadha
- ❖ Mara dufu
- ❖ Siku zote
- ❖ Tele
- ❖ Pomoni
- ❖ Kidogo
- ❖ Mara kwa mara n.k

(5)vielezi vya kutilia mkazo

➤ Husisitiza au kutilia mkazo wa jambo.aidha hukariri jinsi kitendo kilitokea kwa kurejelea.

Mifano:

- ❖ Dhahiri shahiri
- ❖ Liwalo na liwe
- ❖ Uso kwa uso
- ❖ Hali na mali
- ❖ Balaa belua
- ❖ Daima na dawamu
- ❖ Hajijui hajitambui
- ❖ Kwa mapana na marefu
- ❖ Kutwa kucha
- ❖ Kufa na kupona
- ❖ hamu na ghamu
- ❖ fanya juu chini
- ❖ waza na kuwazua
- ❖ Ima fa ima n.k **Zoezi**

Bainisha vielezi vilivyotumiwa kisha ueleze ni vya aina gani

1. Tulikwenda kwa Bi.Mnene asubuhi na mapema.
2. Niliwasili sokoni mapema.
3. Amina na Juma waliahidi kupendana daima dawamu.
4. Mayatima wale walikula wali mwingi wakashiba.
5. Wageni wetu watawasili mtondogoo.
6. Jua huchomoza mashariki.
7. Kazi hii imefanyika kiholela.
8. Alipomaliza kuandika insha, alienda polepole kwa mwalimu.
9. Mwislamu anapaswa kuswali mara tano kwa siku.
10. Mchana kutwa alilala kwa uchovu.
11. Alipofunga bao alibebwa hobelahobela.
12. Utumiaji wa ngamizi haukuwa umekita mizizi zama hizo.
13. Aliloa chepechepe aliponyeshewa.
14. Fanya hima tusije tukachelewa.
15. Mtihani utanza keshokutwa.